TANGAZO LA SERIKALI Na. 493 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA LA MIRADI YA UTEKELEZAJI MPANGO KAZI WA AFYA YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii, itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja la Miradi ya Utekelezajji Mpango Kazi wa Afya ya mwaka 2023 na itaanza kutumika kuanzia tarehe 6 Machi, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuanishwa na Kamishna Mkuu, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari lililoainishwa kwenye Jedwali, litakaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwa niaba ya M/s Amref Health Africa, kwa ajili ya kutumiwa mahususi katika Miradi ya Utekelezaji Mpango Kazi wa Afya kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa ushuru wa bidhaa unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru wa bidhaa utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba Amri hii haikutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa madhumuni tofauti au litahamishwa, kuuzwa, au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidikaka na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 7 Septemba, 2023.

*Tangazo la Serikali Na. 493 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Chassis | Injini |
|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Land Cruiser Hardtop 10 Seater | JTEEB71J80F022157 | 1HZ-1021740 |

Dodoma, MWIGULU LAMECK NCHEMA MADELU
…………………, 2023 *Waziri wa Fedha*